

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO
SHULE YA SEKONDARI BAGAMOYO



Namba za Simu.

Mkuu wa Shule: 0713 405 953

Makamu Mkuu wa Shule:

0762 478 220/0757 114 242

Malezi:0769 397 926/0714251949

Shule ya Sekondari BAGAMOYO

S.L.P 42

Tarehe

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

S.L.P

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BAGAMOYO HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO MKOA WA PWANI MWAKA

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka na atasoma tahasusi ya

Shule ya Sekondari BAGAMOYO ipo umbali wa Kilometa 2.5 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Bagamoyo. Usafiri wa basi unapatikana kutoka kituo cha mabasi cha Bunju Sokoni jijini Dar es salaam mpaka stendi ya mabasi ya Bagamoyo kwa nauli ya Tshs 2000.

Kwa wanaotoka mikoani gari zinapatikana stendi ya Mbezi Luis kwa nauli ya Tshs 4000/= na wale wanaotoka kwenye Mikoa ambayo gari zinapitia Bagamoyo watahuka stendi ndogo ya Kichemchem-Bagamoyo ambapo wanaweza kutumia Usafiri wa pikipiki kwa shilingi 4000 au bajaji kwa shilingi 5000/= mpaka shuleni. Kwa wanaotoka Mbezi Luis au Bunju sokoni, nauli kutoka stendi ya mabasi ya Bagamoyo mpaka Bagamoyo sekondari ni Shilingi 2000/= kwa pikipiki na Shilingi 3000/= kwa bajaji. **NB nauli zinaweza kubadilika**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe Mwisho wa kuripoti ni tarehe Muda wa kuripoti ni kuanzia saa 2:00 Asubuhi mpaka saa 10:30 Jioni, Tafadhali zingatia tarehe na Muda

2.Mambo muhimu ya kuzingatia: -

2.1 Sare za Shule

- i. Kwa wasichana sare ya shule ni sketi mbili rangi ya Maroon iliyokolea mshono wa rinda “box” urefu wa sketi ifunike vifundo vya miguu na kwa wavulana ni Suruali za ‘kaki’ mbili (2) zisizo na marinda (kipimo cha chini kiwe na upana kati ya sm17-18).
- ii. Mashati mawili meupe mapya ya mikono mifupi ya kitambaa cha tetroni kwa wavulana na wasichana. Wasichana wa kiislamu waje na nusu kanzu mbili zisizobana na zivuke magoti na Hijab (Juba) mbili za rangi nyeupe, ziwe ndefu kufikia kifundo cha mikono akisimama.
- iii. Kwa wasichana, viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi au aina ya Juma na Rosa. Na kwa wavulana viatu vyeusi vya kufunga kamba vyenye kisigino kifupi
- iv. Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
- v. Kwa wavulana, Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali usio na nembo ya kihuni wala bakoli nene
- vi. Sweta moja la rangi ya DARK BLUE lenye shingo alama ya V na si vinginevyo.
- vii. Sare ya michezo ni track suit za rangi ya dark blue zenye mistari ya rangi ya bendera ya Taifa pembeni, jezi nyeupe ya Taifa stars na bukta nyeupe na raba za michezo kwa wavulana.
Wasichana watatumia t-shirt nyeupe ya taifa stars na track suit za rangi ya dark blue yenye mistari ya bendera ya taifa pembeni na raba zao ziwe nyeupe.

Nguo za kushindia (Shamba Dress)

- viii. Suruali mbili (2) pana za ‘dark blue’ iliyokolea zisizo na marinda mbele kwa wavulana kwa ajili ya kushindia (kipimo cha chini kiwe na upana kati ya sm17-18).
- ix. Sketi mbili (2) rangi ya ‘Dark blue’ iliyokolea mshono wa rinda box, urefu wa sketi ifunike vifundo vya miguu kwa ajili ya kushindia.
- x. Wasichana waje na suruali mbili (2) rangi ya “dark blue” zisizobana kwa ajili ya kuvaa usiku kujikinga na mbu wakati wa kujisomea.
- xi. T-shirt mbili (2) za rangi ya **Maroon (damu ya mzee)** (maarufu kama form six) isiyo ya maandishi kwa ajili ya kushindia (**T-shirt za shule zenye nembo zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 16,000/= kwa kila moja kwa anayehitaji**)
Kwa waislamu nusu kanzu ya “rangi ya maroon” mbili zinazovuka magoti na hijabu mbili (2) za rangi ya “maroon” zifunike kifundo cha mkono akisimama **NB: wasije na T-shirt kwani watavaa nusu kanzu na hijab.**

1. KWA WAVULANA: Ataripoti shuleni akiwa amevaa suruali ya ‘dark blue’ na Shati nyeupe ya mikono mifupi. Hairuhusiwi kushona suruali ya kubana (model). Suruali za namna hiyo hazitakiwi kabisa shuleni.

2. KWA WASICHANA: Ataripoti shuleni akiwa amevaa sketi ya rangi ya “dark blue” na Shati ya rangi nyeupe ya mikono mifupi.

Kwa waislam avae sketi ya “Dark blue” na nusu kanzu ya “maroon” na Hijabu ya “maroon”.

MUHIMU

Vifaa vya usafi, T-shirt zenye nembo ya shule, tracksuit, jezi, Calculators, magodoro na kava ya ngozi, uniform za shule (shati nyeupe, suruali ya kaki na sketi ya maroon) unaweza kuvipata kwenye duka la shule. (mchanganuo wa bei ya kila kimoja umeambatanishwa)

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -

- i. Madaftari 15 aina ya Counter Book Quire 03
- ii. Karatasi za **A4 Ream** Mbili (2) kwa mwaka, aina ya aOne /double A;
- iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
- iv. Dissecting tray kwa wanafunzi wanaosoma PCB.
- v. Scientific Calculator (fx-991-ES PLUS) kwa wanafunzi wote isipokuwa HKL.
- vi. Stopwatch kwa wanafunzi wanaosoma PCM, PMCs na CBG.
- vii. Graph pads mbili kwa wanafunzi wote isipokuwa HKL.
- viii. Map sheet and Photograph bundle kwa wanafunzi wote wanaosoma Geography.
- ix. Kwa wanafunzi wanaosoma Computer Science wanaruhusiwa kuja na Laptop zao.
- x. Godoro la sponji la futi mbili na nusu kwa futi sita na kava (foronya) yake (**iwe ya ngozi**) **NB: yanapatikana shuleni**
- xi. Mashuka mawili (2) ya rangi ya pink na moja la kujifunika, chandarua 1 nyeupe na mto wa kulalia.
- xii. Nguo za ndani za kutosha. NB kwa wavulana aje na BOXER zisizopungua 10
- xiii. Vyombo vya chakula (Sahani yenye vyumba na container yenye mfuniko) siyo vya plastiki Pamoja na kikombe cha chai
- xiv. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.
- xv. Aje na tochi kwa ajili ya tahadhari kwa wakati wa usiku (Isiwe ya kuchaji kwa umeme)
- xvi. Aje na ndala kwa kuogea na Sandals za kushindia (Zisiwe Crooks au zenye soli nene)
- xvii. Aje chupa safi kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
- xviii. Aje na Box file kwa ajili ya Portfolio.
- xix. Mwanafunzi aje na kadi ya Bima ya afya kama anayo au aje na Tsh. 50,400 pamoja nan amba ya NIDA kwa ajili ya kukatia Bima ya Afya shuleni. Hii ni lazima kwa wanafunzi wote.

MAHITAJI KWA MAKUNDI: Mwanafunzi pia atapaswa kuja na vifaa vifuatavyo kulingana na mchepuo wake.

EBuAc/HGE	PCB	PCM	CBG	PMCs	HKL	EGM	BuAcM
Dawa ya kusafishia vyoo lita tano aina ya LIT	Jembe na mpini wake	Reki	Soft broom	Mkasi wa kukatia fensi ya maua	Panga Soft broom	Hand broom	Spade
Mfagio wa wima wa chelewa	Soft broom	Soft broom	Hard broom	Squeezer (rubber)	Mfagio wa wima wa chelewa	Soft broom	Hand broom

	Squeezer	Mfagio wa wima wa chelewa	Sabuni ya kunawia lita tano aina ya TARMOL		Slesha/Kwanja	Slesha	Mfagio wa wima wa chelewa
--	----------	---------------------------	--	--	---------------	--------	---------------------------

2.3 Michango mbalimbali

Na	Aina ya Mchango	Kiasi	Maelezo
1.	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=	Kwa mwaka
3.	Tahadhari	5,000/=	Mara moja
4.	Nembo	5,000/=	
5.	Kitambulisho cha Shule	5,000/=	
	Jumla	80,000/=	

Malipo yote yafanyike kwenye akaunti ya shule.

Jina la akaunti; Bagamoyo Secondary School. Namba ya akaunti; A/C 21001200044, Benki ya NMB.

3.Viambatisho, Fomu Muhimu na maagizo mengine.

- Uchunguzi wa Afya (Medical Examination) utafanywa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali.
- Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
- Passport size moja (1) kwa kila mzazi/mlezi wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za Simu.
- Picha zake sita (5) za passport size ziwe na 'background ya blue' na vipimo vya sm.4 kwa 4 na awe amevaa shati jeupe wakati wa kupiga picha hizo.

4.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu–TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

4.1 Sheria na Kanuni za Shule

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima. Mwanafunzi **atapaswa kusimama** anapomsalimia mwalimu au yeyote anayemzidi umri.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- Kushiriki kwa kikamilifu na kwa utulivu masomo ya usiku (Preparation);
- Kuwahi na kuhudhuria katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- Kutunza mali za shule;
- Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;

11. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini awapo shuleni.
12. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na mapambo, urembo, mafuta yenye harufu kali au manukato ya aina yoyote.

4.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

- i. Wizi;
- ii. Kutohudhuria masomo
- iii. Utoro;
- iv. Kugoma, kuchochea na kuhamasisha mgomo au kuvuruga amani au kusababisha kuvuruika kwa amani na usalama wa watu shuleni;
- v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- vi. Kupigana; vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya; viii. Uvutaji wa sigara;
- vii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuo au kuolewa;
- viii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- ix. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- x. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi na viambatanisho vyake kama chaja, laini, earphones katika mazingira ya shule;**
- xi. Kudharau Bendera ya Taifa;
- xii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
- xiii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
- xiv. Kukataa adhabu halali.

MUHIMU:

- ✚ **Mwanafunzi HAPASWI KUJA NA SIMU/AU KIFAA CHOCHOTE KINACHOHUSIANA NA SIMU shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Pia mwanafunzi haruhusiwi kuja na kifaa chochote kinachotumia umeme.**
- ✚ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ✚ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule (Msiba au Ugonjwa). Mzazi/mlezi atalazimika kumfuata na kumrudisha mwanae shuleni.**
- ✚ **Mzazi/mlezi anashauriwa kufika shuleni mara kwa mara katika siku za kazi ndani ya muda wa kazi ili kufuatilia maendeleo ya mwanae kitaaluma na kimwenendo na atapaswa kuripoti ofisini kabla hajakutana na mwanaye kila anapofika.**
- ✚ **Siku pekee za kutembelea wanafunzi (Visiting day) kwa muhula wa kwanza ni Jumamosi ya mwisho ya mwezi wa kumi na kwa muhula wa pili ni jumamosi ya mwisho ya mwezi wa pili.**
- ✚ **Kila mwanafunzi aweke alama/label inayoonekana kwenye sare na mali zake binafsi.**
- ✚ **Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wagonjwa. Pia ni marufuku kuja na chakula cha aina yoyote hapa shuleni.**
- ✚ **Mwanafunzi ahakikishe anakuja na sanduku la chuma/bati (tranka) moja linalotosha kutunzia vitu vyake.**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NB: KWA MAWASILIANO SHULENI TUMIA NAMBA ZIFUATAZO: -


> Mkuu wa shule : 0713 405 953

- Makamu Mkuu wa Shule: 0762 478 220/0757 114 242
- Mwandamizi Taaluma : 0769 260 151
- Ofisi ya Malezi: 0769 397 926/ 0787 148 857/0714251949

Kwa ajili ya ufuatiliaji zaidi wa matokeo ya mwanao, tembelea tovuti yetu ambayo ni www.bagamoyo.sc.tz

Pia tuandikie kupitia e-mail yetu ambayo ni bagamoyosecondary@gmail.com

KARIBU SANA BAGAMOYO SEKONDARI



TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. i) Jina kamili la mwanafunzi.....Me/Ke
- ii) Tarehe ya kuzaliwa..... mwezi.....mwaka.....
- iii) Shule uliyotoka kidato cha Nne;.....
2. Je wazazi wote wapo hai? Ndiyo / hapana.....
- a) Na kama hapana nani yuko hai

TAARIFA ZA WAZAZI/ WALEZI

- Jina la Baba..... Kazi yake
- Anuani yake: Makazi yake.....Simu :.....
- Jina la Mama..... Kazi yake
- Anuani yake: Makazi yake.....Simu:.....
- b) Kama unalelewa na mlezi asiye mzazi wako;
- Jina la mlezi wako (majina matatu).....
- Uhusiano na mlezi wako (kaka, dada, n.k)..... Kazi yake.....
- Anwani yake..... Makazi yake:Simu.....

AFYA.

- a) Je una ulemavu wa viungo? Ndiyo /hapana.....
- b) Kama ndiyo taja aina ya ulemavu.....
3. Orodhesha majina ya ndugu watatu (nje ya uliowataja hapo juu) ambao wanaweza kuitwa kwa dharura.

Na.	JINA KAMILI	UHUSIANO	ANUANI YA ANAKOISHI	NAMBA YA SIMU	PICHA
1					
2					
3					

4. Uthibitisho wa taarifa iliyotolewa;
- Mimi (jina la mwanafunzi)nathibitisha
- kwamba maelezo niliyotoa ni ya KWELI na endapo itathibitika kuwa nimedanganya hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.
- Tarehe..... Sahihi.....
5. Jina na sahihi ya mzazi/mlezi : Jina..... Sahihi.....
6. **Jina na sahihi ya mwenyekiti wa kijiji/Afisa Mtendaji/serikali za mitaa/kitongoji**
- Jina..... Sahihi..... Muhuri.....**

AHADI YA KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi.....

Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **Shule ya Sekondari Bagamoyo kidato cha tano** mchepuo.....mwaka.....ninaipokea na kuikubali nafasi niliyopewa.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili yangu binafsi, familia yangu na Taifa langu la Tanzania.

Ninaamini kuwa vitendo vyovyote vinavyosababisha uzembe katika kufanikisha

Makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, Shule yangu na familiya yangu na kwangu pia.

Hivyo ninaahidi kuwa;

1. Nitasoma kwa bidii na kufanya mitihani na majaribio yote ili kufikia malengo ya kufanya vizuri katika masomo.
2. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zinatolewa mara kwa mara.
3. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapa shuleni na nje ya shule.
4. Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni, na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za shule.

Sahihi ya mwanafunzi:Tarehe:

Sehemu ya mzazi/mlezi.

Mimi.....ninakubali mtoto wangu

kupata na kupokea nafasi katika shule ya Sekondari Bagamoyo kidato cha tano mwaka

Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.

Ninakupakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.

Anwani yangu ya kudumu ni.....

.....

.....

Namba ya simu.....

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi nitajulisha shule kwa maandishi.

Sahihi:Tarehe:.....

PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a medical Officer in respect of all form I and 5 entrants)

Student's full name:

Student's age: Form.....

(To be completed by a government medical officer):

I have examined the above named student and consider that he/she is fit/unfit for full time studies.

- 1) Eyesight.....
- 2) Hearing.....
- 3) Speech.....
- 4) Limbs.....
- 5) Venereal disease.....
- 6) Leprosy.....
- 7) Epilepsy.....
- 8) Neurosis.....
- 9) Asthma.....
- 10) T.B.....
- 11) Pregnancy.....
- 12) Diabetes.....
- 13) Ulcers.....
- 14) Other.....

MEDICAL OFFICER'S COMMENTS:

.....
.....
.....

Name.....Signature.....Date.....Stamp:

Station.....Designation.....

NB: I request this form to be returned to the school

VIFUATAVYO NI BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI

Mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu kulingana na masomo yake kwa kufuata mchanganuo ufuatao.

<p style="text-align: center;">CHEMISTRY</p> <ol style="list-style-type: none"> Modern's ABC of Chemistry by Dr. s. Jauhar (2017-2018) for class XI & XII part I & II Essentials of Physical Chemistry class XI & XII by Chand Advanced Physical Chemistry by Ngaiza Lusima (2014) Conceptual Chemistry for Class XI by S.K JAIN Comprehensive Chemistry volume I class XII by Dr. N.K. Verma, S.K. Khanna & Dr. B. Kapila Advanced Organic Chemistry by Arun Bahl, S. Chand 	<p style="text-align: center;">HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI</p> <ol style="list-style-type: none"> HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI KIDATO CHA TANO, TIE 	<p style="text-align: center;">HISTORY</p> <ol style="list-style-type: none"> Advanced Learning World History by Idrisa Msuya book 1 & 2 Essentials in Advanced level History paper 1 & 2 by Saleh Yasin Advanced Level History 1 & 2 by K. Shibitali Medieval Ages paper 2 by M Mavunde 	<p style="text-align: center;">KISWAHILI</p> <p style="text-align: center;">a) USHAIRI</p> <ol style="list-style-type: none"> Fumbo linaloelea Nyambari C.M.Nyangwine Malenga wa ziwa kuu Wallah Bin Wallah Andamo, Msafari safarini M.Khelef Ghassani Wosi awa Baba Ahmed Mohamed Amanzy <p style="text-align: center;">(b) RIWAYA</p> <ol style="list-style-type: none"> Dunia Uwanja wa fujo.E. Kezila habi Mirathi ya hatari C.G. Mng'ongo Siti binti saad shaban Robert Ua la faraja W.E.Mkufya
<p style="text-align: center;">ADVANCED MATHEMATICS</p> <ol style="list-style-type: none"> Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Schools form five by TIE Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Schools form Six by TIE Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools Form V & VI by Septine I. Sillem (2015) Conceptual Advanced Mathematics for Secondary Schools Form V & VI by P. L. Mayombya 	<p style="text-align: center;">BASIC APPLIED MATHEMATICS</p> <ol style="list-style-type: none"> Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools form V by Septine I. Sillem, 2014 Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools form VI by Septine I. Sillem, 2014 Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools form five and Six by TIE 	<p style="text-align: center;">GEOGRAPHY</p> <ol style="list-style-type: none"> Integrated Approach in Geography by David Waugh (2009) 3rd edition A Comprehensive Approach in Physical Geography by D.T. Msabila (2018) Practical Geography by Zisti Kamili 2nd Edition 2016 Complementary Physical Geography for secondary school by O. Mpalaki & F. Lighuda Affordable Edition for Advanced learners by Zist Kamili Fundamental in Advanced level practical Geography by Avelius T. Thobias Practical Geography for Advanced secondary school by Tanzania institute of education Physical Geography for Advanced secondary school by Tanzania institute of education 	<p style="text-align: center;">(c) TAMTHILIYA</p> <ol style="list-style-type: none"> Mukwawa wa uhehe - M.M.Mulokozi Shujaa Mirambo E.Mbogo Usaliti Mjini F.Imbuga

ENGLISH LANGUAGE	ECONOMICS	PHYSICS	KISWAHILI 1 & 2
<ol style="list-style-type: none"> 1. .Advanced level English Language 1 by Ndambo, NNP Publishers 2. Advanced English Language form 5&6 by James John, Oxford university press 3. English language for secondary school, language and use form 5&6 by TIE 4. Advanced level English language form 5&6 by Nicholous Asheli 5. Oxford Advanced learners Dictionary by Oxford university press 6. Animal farm – by George orwell 7. Chasing the leopard finding the lion by Juke Wakeman 8. The opportunist by N.Nyangwine 9. The Horizon Unveiled By Fellowes mwaisela. 10. The government inspector By Nikolai V. Gogol 11. An Enemy of the people By H.IBSEN 12. A taste of Heaven – By Farouk Topan 13. Summons poems from Tanzania – Richard S. Mabala 14. Poets of Africa Lament of silent & other poems – By Jared Angira 	<ol style="list-style-type: none"> 1.Economics 1 & 2 by Tayebwa Mgisha 2.Modern Economics Theory by Dewelt. 3. Essential Economics 1&2 by Odhiambo. 4. Modern Economics 20th Edition by Ahuja 5. Comprehensive of Economics Questions and Answers by Tayebwa. <p style="text-align: center;">BIOLOGY</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Biological science(D) Taylor, N.Green 2. Advanced Biology, (By C.J. Cleggy) 3. New understanding Biology (Glenn and Susan Toole 4. Advanced Biology Principles and application 5. Advanced Biology for you (Garreth Williams) 6. Dissection manual (Rowett) 7. Advanced Biology form VI (Rivehumbiza) 	<ol style="list-style-type: none"> 1. Physics for Advanced level secondary schools, students book Form five by TIE 2. Physics for Advanced level secondary schools, students book Form six by TIE 3.Principles of physics for class XI, V.K Mehta, S. Chand 4. Principles of physics for class XII, V.K Mehta, S. Chand 5. Modern ABC of physics for class XI part I & II by Satish K. Gupta 6. Modern ABC of physics for class XII part I & II by Satish K. Gupta 7.Essentials of Physics part one by Nicholaus M.Z 	<ol style="list-style-type: none"> 1.Nadharia ya Fasihi by Kilangi Enock Lucas, Zenur Printers Dsalaam 2019 2.Tahakiki ya Kiswahili by Kilangi Enock Lucas, Zenur Printers Dsalaam 2019 3.Kiswahili 1 kwa Shule za Sekondari kidato cha 5 & 6 by Kilangi Enock Lucas, Zenur Printers Dsalaam 2019 KISWAHILI 1 & 2 4.Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) sekondari na vyuo by Y.M Kihore, Massamba na Msanjila, TUKI 5.Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na mbinu by H.J Mwansoko, Mekacha na Mtesingwa, TUKI <p style="text-align: center;">ACCOUNTANCY</p> <ol style="list-style-type: none"> 1.Advanced Accounting I & II, 10th edition by Frank Wood 2. Accountancy for Advanced secondary school students book form v By Tanzania Institute of Education. 3.Advanced Accountancy volume I & II by S.N.Maheshwani <p style="text-align: center;">COMMERCE</p> <ol style="list-style-type: none"> 1.New Trend in Commerce by AbdulLatif Katende 2.Textbook of Commerce by Dina Kamasanyu 3.Simplified Commerce by Saleemi

NB: ZIFUATAZO NI BEI ZA VIFAA AMBAVYO VINAWEZA KUPATIKANA MAENEO YA HAPA SHULENI

KIFAA	BEI
Godoro - 1	52,000/=
Foronya/ kava ya godoro (ya Ngozi) -1	32,000/=
T-shirt yenye nembo ya shule - 1	16,000/=
Vifaa vya usafi (Soft broom, hard broom, squizzer, chelewa, hand broom, na fyekeo).	Kila kimoja (@)3500/=
Jembe lenye mpini	9,000/=
Scientific Calculator fx-991 - 1	30,000/=
Rimu (aOne)	15,000/=
Lab coat -1	17,000/=
Suruali -1	25000
Sketi - 1	30000
Shati -1	12000